ZAN SECURITIES

LICENSED DEALER OF DSE | INVESTMENT ADVISOR | FUND MANAGER

TAARIFA YA MWAKA YA MFUKO WA UWEKEZAJI WA

TIMIZA FUND

KWA MWAKA UNAOISHIA 2025

ZAN SECURITIES LIMITED

TAARIFA YA MWAKA YA MFUKO WA UWEKEZAJI WA TIMIZA
(TIMIZA FUND)

KWA MWAKA UNAOISHIA
31 DESEMBA 2025

YALIYOMO

1. TAARIFA YA MWENYEKITI WA BODI 6
2. TAARIFA YA MWANGALIZI WA MFUKO 8
3. TAARIFA YA MKAGUZI WA MFUKO 11
4. TAARIFA YA HESABU ZA MFUKO 14
5. TAARIFA YA MENEJA KUHUSU UWEKEZAJI 18
6. AZIMIO LA MKUTANO MKUU 22

ZAN SECURITIES LMITED
MKUTANO MKUU WA KWANZA WA WAWEKEZAJI WA MFUKO WA TIMIZA (TIMIZA FUND)

SIKU YA JUMAMOSI, TAREHE 7 MACHI 2026 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA KIMATAIFA WA JULIUS NYERERE
DAR ES SALAAM

RATIBA NA AJENDA ZA MKUTANO

MTIRIRIKO WA SHUGHULI

NA	MUDA	SHUGHULI	WAHUSIKA
1	02.30 - 03.40	Kuwasili kwa Wajumbe na Kujiorodhesha	Wajumbe/Utawala
2	03.40 - 03.50	Matangazo na Shughuli za Utawala	MC/Utawala
3	03.50 - 04.00	Kuthibitisha Akidi na Kufungua Mkutano	Afisa Mtendaji Mkuu
4	04.00 - 04.15	Utambulisho (Wajumbe wa Bodi, Menejimenti, Wadau Waalikwa na Watoa Huduma wa Mfuko)	Mwenyekiti wa Bodi
5	04.15 - 04.30	Taarifa ya Mwenyekiti wa Bodi	Mwenyekiti wa Bodi
6	04.30 - 05.15	**Kupokelewa kwa Taarifa ya Mwaka:**	
		Taarifa ya Mwangalizi wa Mfuko	Benki ya Mwanga Hakika
		Taarifa ya Mkaguzi wa Hesabu	Mazars
		Taarifa ya Hesabu za Mfuko	Meneja wa Fedha na Uwekezaji
		Taarifa ya Meneja Kuhusu Uwekezaji	Meneja wa Ushauri
7	05.15 - 06.00	Kipindi cha Maswali na Majibu	Mwenyekiti/ Watendaji
8	06.00 - 06.15	**Azimio la Mkutano Mkuu** na Kufunga Mkutano	Mwenyekiti wa Bodi

TAARIFA YA MWAKA MFUKO WA TIMIZA FUND

1. TAARIFA YA MWENYEKITI WA BODI

TAARIFA YA MWENYEKITI

Ndugu Wawekezaji,

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi ya ZAN Securities, ambaye ni Meneja wa Mfuko wa Timiza Fund, ninafuraha kuwakaribisha nyote katika Mkutano Mkuu wa Kwanza wa Mfuko wa Timiza (TIMIZA FUND). Tunawashukuru kwa kutenga muda wenu kuhudhuria mkutano huu muhimu, ambao utajadili maendeleo ya Mfuko kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba 2025.

Ndugu Wawekezaji, ninaamini mmekuwa mkifuatilia maendeleo ya Mfuko wa Timiza, na kwamba mmeipokea na kuisoma taarifa ya Mfuko kwa kipindi kilichoishia tarehe 31 Desemba 2025. Ninafuraha kuwajulisha kuwa utendaji wa Mfuko katika kipindi hicho ulikuwa mzuri sana. Faida kwa wawekezaji ilikuwa kubwa ikilinganishwa na kigezo linganifu (performance benchmark).

Faida ya Mfuko ilifikia asilimia 15.032 kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2025. Faida hii inaendana na mwenendo wa soko la fedha na ni kubwa kuliko kigezo linganifu cha asilimia 11.4, ambacho ni kiwango cha hati fungani ya miaka kumi.

Katika kipindi kilichoishia Desemba 2025, thamani halisi ya Mfuko iliongezeka na kufikia shilingi bilioni 27.1, ikilinganishwa na shilingi bilioni 14.4 katika kipindi kilichoishia tarehe 31 Desemba 2024.

Ongezeko hili limetokana na utendaji mzuri wa uwekezaji uliowezesha kupatikana kwa faida, matumizi ya teknolojia katika kurahisisha miamala ya uwekezaji, kuimarika kwa imani ya wawekezaji na hivyo kuongezeka kwa ushiriki wao katika Mfuko, pamoja na kuongezeka kwa uelewa kuhusu manufaa ya kuwekeza kupitia mifuko ya uwekezaji wa pamoja.

Aidha, ukuaji wa Mfuko umechangiwa pia na ongezeko la idadi ya wawekezaji, ambapo hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2025, jumla ya wawekezaji ilifikia 3,840.

Vilevile, kutokana na ukuaji huo, Mfuko umeweza kupata ziada (surplus) itakayowezesha kutolewa kwa gawio la shilingi kumi kwa kila kipande kwa wawekezaji waliochagua mpango wa kupokea gawio. Kwa wawekezaji waliopo kwenye mpango wa kuwekeza upya (reinvestment), wataongezewa vipande kulingana na kiasi hicho, kama ilivyoainishwa katika Waraka wa Toleo.

Mazingira katika Masoko ya Fedha

Ndugu Wawekezaji, maendeleo ya Soko la Mitaji na Dhamana, ambalo utendaji wake hupimwa kwa kuangalia mabadiliko ya fahirisi ya soko (Tanzania Share Index), yalionesha mwenendo mzuri. Katika mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2025, fahirisi iliongezeka kwa asilimia 24.69, kutoka 4,618.78 tarehe 31 Desemba 2024 hadi 5,759.41 tarehe 31 Desemba 2025.

Ongezeko hili ni kubwa zaidi ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 6.90 lililorekodiwa kati ya tarehe 31 Desemba 2023 na 31 Desemba 2024. Hii inaonesha kuwa, katika mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2025, bei za hisa kwa ujumla ziliongezeka kwa kiwango kikubwa zaidi kuliko mwaka uliotangulia.

Tunamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na Serikali kwa ujumla, kwa kuendelea kusimamia na kuweka mazingira bora ya biashara na uwekezaji nchini.

Aidha, tunaiomba Serikali na vyombo vya usimamizi wa masoko kuendeleza juhudi za kuboresha mazingira ya masoko, ili wawekezaji waendelee kunufaika na ongezeko la thamani ya uwekezaji pamoja na kukuza kipato chao.

Matarajio

Ndugu Wawekezaji, katika kipindi kilichoishia Desemba 2025, ZAN Securities imepata mafanikio makubwa zaidi ya ilivyotarajiwa, ikiwa ni pamoja na kuanzisha Mfuko wa Timiza, ambao unatoa pato shindani katika soko.

Katika siku zijazo, ZAN Securities itaendelea kutekeleza mipango yake ya kimkakati, ikiwemo elimu ya kuboresha mifumo na huduma kwa wawekezaji, pamoja na kubainisha fursa nyingine za kibiashara kwa manufaa ya wawekezaji na wadau wengine. Aidha, itaendelea kuimarisha mfumo wa uendeshaji wa mifuko ili uwe wa kisasa zaidi na kuhakikisha wawekezaji wanapata faida shindani inayoendana na hali ya soko. Kwenye hili ZAN Securities iko wazi kupokea mawazo ya juu ya kuboresha Mfuko ili uweze kutoa huduma nzuri Zaidi.

Shukrani

Ndugu Wawekezaji, katika kuhitimisha taarifa yangu, napenda kuwashukuru nyote kwa ushirikiano na imani yenu kwa ZAN Securities na Mfuko wa Timiza katika kipindi chote kilichoishia tarehe 31 Desemba 2025.

Kwa namna ya kipekee, napenda kuishukuru Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa kuendelea kuweka mazingira bora ya uwekezaji katika soko la mitaji; Soko la Hisa la Dar es Salaam; Mwangalizi wa Mifuko ambaye ni Benki ya Mwanga Hakika; Mkaguzi wa Mfuko, Forvis Mazars; pamoja na Mwanasheria wa Mfuko, MM Attorneys, kwa kuwezesha mfuko kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa.

Aidha, napenda kuwashukuru kwa ujumla mawakala wote wa soko la hisa, wenzangu Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi, wafanyakazi wa ZAN Securities, na wadau wote ambao wameendelea kuiwezesha ZAN Securities kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na weledi.

Napenda kuwahakikishia kuwa Mfuko wa Timiza utaendelea kufanya vizuri zaidi, na kwa uaminifu wa hali ya juu, na ni matumaini yangu kuwa ushirikiano huu utaendelea kwa manufaa ya wawekezaji wetu na maendeleo ya Soko la Mitaji na

Abdisalaam Issa Khatibu

Mwenyekiti wa Bodi

2. TAARIFA YA MWANGALIZI WA MFUKO

MWANGA HAKIKA BANK

TAARIFA YA MWANGALIZI WA MFUKO WA TIMIZA KWA WAWEKEZAJI

Hili ni toleo lililotafsiriwa la ripoti ya Mwangalizi wa mfuko iliyosainiwa katika toleo la Kiingereza

1. UTANGULIZI

Ripoti hii ya Mwangalizi wa mfuko wa Timiza imeandaliwa kwa ajili ya Mkutano Mkuu wa Mwaka (AGM) wa Mfuko wa TIMIZA. Ripoti hii inatoa muhtasari wa shughuli za mwangalizi na kutoa uhakiki juu ya uangalizi wa dhamana za uwekezaji, uzingatiaji wa kanuni, na uzingatiaji wa Hati ya Makubaliano (Trust Deed) na Mkataba wa uangalizi kulingana na Kanuni za Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja za CMSA (Tanzania).

2. WAJIBU NA MAJUKUMU YA MWANGALIZI

Benki ya Mwanga Hakika Ltd, kama mwangalizi wa mfuko, imetekeleza wajibu na majukumu makuu katika kipindi husika kama ifuatavyo:

- **i.** Kuchukua chini ya uangalizi mali zote za mfuko na kuishikilia kwa niaba ya wamiliki wa vipande kwa mujibu wa masharti ya Hati ya makubaliano na kuhakikisha kuwa fedha taslimu na rasilimali zinazosajiliwa zinashikiliwa au kusajiliwa kwa jina la Mfuko wa Timiza
- **ii.** Kuwajibika kwa kitendo chochote ambacho ni kinyume na utaratibu wa wakala yeyote ambaye uwekezaji umefanyika kupitia kwake;
- **iii.** Kuchukua tahadhari inayostahili kuhakikisha kuwa uuzaji wa awali, uuzaji wa kawaida, ununuzi (repurchase) wa vipande unaofanywa na mfuko unatekelezwa kwa mujibu wa masharti ya Hati ya makubaliano;
- **iv.** Kuchukua tahadhari inayostahili kuhakikisha kuwa njia zinazotumiwa na Meneja katika kukokotoa thamani ya vipande zinajitosheleza kuhakikisha kuwa bei za uuzaji na ununuzi zinatolewa kwa mujibu wa masharti ya Hati ya makubaliano;
- **v.** Na majukumu mengine kama yalivyoainishwa katika Hati ya makubaliano na waraka wa toleo wa Mfuko wa TIMIZA.

3. JALADA LA DHAMANA ZA MFUKO KUFIKIA TAREHE 31 DESEMBA 2025

Mwangalizi anathibitisha uangalizi salama na uorodheshwaji sahihi wa rasilimali zote za Mfuko. Hakuna hasara, uhamishaji usioidhinishwa, au hitilafu zilizotokea katika kipindi cha ripoti.

Jalada la dhaman za mfuko kufikia tarehe 31 Desemba 2025 ni kama ifuatavyo:

3.1. Fedha Taslimu

Katika kipindi kilichoishia tarehe 31 Desemba 2025, fedha taslimu zinajumuisha:

Maelezo	Kiasi (TZS)
Salio la Benki – Akaunti ya Makusanyo	439,049,815
Salio la Benki – Akaunti ya 'Call'	4,500,942,708
Jumla ya Fedha Taslimu	**4,939,992,523**

3.2. Uwekezaji katika Dhamana za Serikali

Maelezo	Kiasi (TZS)
Hati Fungani ya Serikali – Miaka 25 (Toleo 639), Thamani TZS 100M	104,169,863
Hati Fungani ya Serikali – Miaka 20 (Toleo 498), Thamani TZS 500M	480,623,426
Hati Fungani ya Serikali – Miaka 7 (Toleo 562), Thamani TZS 201M	185,810,735
Hati Fungani ya Serikali – Miaka 25 (Toleo 617), Thamani TZS 250M	265,778,424
Hati Fungani ya Serikali – Miaka 25 (Toleo 675), Thamani TZS 500M	597,331,274
Hati Fungani ya Serikali – Miaka 15 (Toleo 551), Thamani TZS 20B	18,958,522,824
Jumla ya Uwekezaji katika Dhamana za Serikali	**20,592,236,546**

3.3. Hisa

Hisa	Kiasi (TZS)
CRDB – Hisa 1,000,000	1,510,000,000.00
NMB – Hisa 76,000	639,160,000.00
Jumla ya Hisa	**2,149,160,000.00**

3.4. Taarifa Nyingine kuhusu Mfuko

Maelezo	Kiasi (TZS)
Mauzo ya vipande (Sales)	28,008,657,166
Unuzuzi wa Vipande (Repurchase)	(4,367,873,701)
Mabadiliko ya thamani ya mfuko	23,640,783,465
Jumla ya Thamani ya Vipande (AUM) Tarehe 31 Desemba 2025	27,167,893,463

4. UZINGATIAJI WA TARATIBU

Mwangalizi alifuatilia uzingatiaji wa kanuni, mipaka ya uwekezaji, mahitaji ya ukwasi kulingana na Hati ya Makubaliano na kanuni za CMSA. Shughuli zote zilizingatia Hati ya Makubaliano ya Mfuko wa TIMIZA na mahitaji ya kisheria. Katika kipindi kilichoishia tarehe 31 Desemba 2025 hakuna ukiukwaji ulioonekana, na Mwangalizi atahakikisha Meneja wa Mfuko anatii taratibu na kanuni zinazohusika.

5. USIMAMIZI WA MIAMALA YA MFUKO

Ununuzi na uuzaji wa vipande vilifanyika kulingana na Thamani Halisi ya mfuko (NAV) inayohusika na kukamilika ndani ya muda unaotakiwa. Mapato yote—ikiwa ni pamoja na riba na malipo ya kuponi—yalipokelewa na kuwekwa kwa usahihi. Ada na gharama zilizotozwa kwenye Mfuko zilipitiwa na kuidhinishwa ipasavyo.

6. MAONI YA MWANGALIZI

Kama Mwangalizi wa Mfuko wa TIMIZA, jukumu letu ni kuhakikisha kuwa Meneja wa Mfuko anatekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Hati ya makubaliano katika kuhakikisha kuwa maslahi ya wamiliki wa vipande yanalindwa.

Katika kutekeleza jukumu hili, miongoni mwa mengine, jukumu la Mwangalizi ni pamoja na kutunza mali zote za mfuko kwa niaba ya wamiliki wa vipande, kuhakikisha kuwa taratibu zinazotumiwa na Meneja kukokotoa Thamani Halisi ya Mfuko (NAV) inajitosheleza na iko kwa mujibu wa Hati ya Makubaliano na kuhakikisha kuwa uwekezaji unaofanywa na Meneja unaendana na malengo ya uwekezaji yaliyowekwa. Katika kipindi hicho Kufikia tarehe 31 Desemba 2025, sisi, kama Mwangalizi wa Mfuko wa TIMIZA, tumekuwa tukifuatilia kwa karibu utendaji wa meneja wa mfuko wa TIMIZA na kufanya tathmini ya uwekezaji wa mfuko

Katika suala hili, tunapenda kuthibitisha kuwa shughuli za uwekezaji chini ya mfuko wa Uwekezaji wa TIMIZA na wajibu wa Meneja wa Mfuko (ZAN SECURITIES LTD) zimekuwa kwa mujibu wa taaratibu na Hati ya Makubaliano. Vile Vile tunathibitishwa kuwa maslahi ya wamiliki wa vipande chini ya mfuko wa TIMIZA yanalindwa ipasavyo na meneja amesimamia Mfuko kwa mujibu wa masharti ya Hati ya Makubaliano

7. HITIMISHO

Kama Mwangalizi , tunathibitisha katika kuhakikisha usalama, uwazi, na usimamizi sahihi wa rasilimali za Mfuko wa TIMIZA. Tunashukuru kwa imani ya wawekezaji na tunatarajia kuendelea kwa ushirikiano na Meneja wa Mfuko.

Kwa na kwa Niaba ya

Mwanga Hakika Bank Ltd,

Jagjit Singh
Mkurugenzi Mtendaji

Chomete Hussein
Mkuu wa Fedha

3. TAARIFA YA MKAGUZI WA MFUKO

TAARIFA YA MKAGUZI KUHUSU MUHTASARI WA HESABU ZA MFUKO WA TIMIZA

Hili ni toleo lililotafsiriwa la ripoti ya Mkaguzi iliyosainiwa katika toleo la Kiingereza

Maoni

Tumekagua taarifa za fedha za Mfuko ya Uwekezaji wa Pamoja wa TIMIZA FUND, kama zilivyoainishwa kwenye kurasa za 14 hadi 17. Hizi zinajumuisha taarifa ya hali ya kifedha kufikia tarehe 31 Desemba 2025; taarifa ya faida au hasara na mapato mengine jumuishi ; taarifa ya mabadiliko ya mali halisi inayotokana na wamiliki wa vipande; taarifa ya mtiririko wa fedha kwa kipindi cha miezi 19 kilichoishia tarehe hiyo; na maelezo ya ziada yanayoambatana, ikiwa ni pamoja na muhtasari wa sera muhimu za kihasibu.

Kwa maoni yetu, taarifa za fedha zinatoa taswira ya kweli na ya haki ya hali ya kifedha ya Mfuko kufikia tarehe 31 Desemba 2025, na utendaji wake wa kifedha na mtiririko wa fedha kwa kipindi kilichoishia tarehe hiyo, kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Kuripoti Taarifa za Fedha (IFRS Accounting Standards) na Kanuni za Masoko ya Mitaji na Dhamana (Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja) za mwaka 1997.

Msingi wa Maoni

Tulifanya ukaguzi wetu kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISAs). Majukumu yetu chini ya viwango hivyo yameelezwa zaidi katika sehemu ya ripoti yetu inayohusu Majukumu ya Mkaguzi katika Ukaguzi wa Taarifa za Fedha. Sisi ni huru dhidi ya Mfuko na Meneja wa Mfuko kwa mujibu wa Kanuni za Maadili za Kimataifa za Wahasibu (IESBA Code) pamoja na mahitaji ya kimaadili ambayo ni muhimu katika ukaguzi wetu wa taarifa za fedha nchini Tanzania, na tumetimiza majukumu yetu mengine ya kimaadili kwa mujibu wa mahitaji haya. Tunaamini kwamba ushahidi wa ukaguzi tuliopata ni wa kutosha na unaofaa kutoa msingi wa maoni yetu.

Taarifa Nyingine

Wakurugenzi wa Meneja wa Mfuko wanawajibika kwa taarifa nyinginezo. Taarifa hizo nyingine zinajumuisha maelezo yaliyomo kwenye Ripoti ya Mwaka ya Mfuko na Taarifa za Fedha kwa kipindi cha miezi 19 kilichoishia tarehe 31 Desemba 2025, lakini haijumuishi taarifa za fedha na ripoti yetu ya ukaguzi. Maoni yetu juu ya taarifa za fedha hayahusu taarifa hizo nyingine na hatutoi aina yoyote ya hitimisho la uhakika juu yake.

Majukumu ya Wakurugenzi wa Meneja wa Mfuko kwa Taarifa za Fedha

Wakurugenzi wa Meneja wa Mfuko wanawajibika kwa uandaliaji wa taarifa za fedha zinazotoa taswira ya kweli na ya haki kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Kuripoti Taarifa za Fedha (IFRS) na kwa namna inayohitajika na Kanuni za Masoko ya Mitaji na Dhamana za mwaka 1997, na kwa udhibiti wa ndani kama Wakurugenzi wanavyoona ni muhimu ili kuwezesha uandaliaji wa taarifa za fedha ambazo hazina makosa makubwa, yajitokezayo kwa udanganyifu au makosa.
Katika kuandaa taarifa za fedha, Wakurugenzi wa Meneja wa Mfuko wanawajibika kutathmini uwezo wa Mfuko wa kuendelea kuwepo, wakibainisha, kadiri inavyostahili, mambo yanayohusiana na uendelevu wa biashara isipokuwa kama Wakurugenzi wana nia ya kufunga Mfuko au kusitisha shughuli zake.

Majukumu ya Mkaguzi katika Ukaguzi wa Taarifa za Fedha

Malengo yetu ni kupata uhakika wa kutosha kuhusu taarifa za fedha kama hazina makosa makubwa, iwe kwa sababu ya udanganyifu au makosa, na kutoa ripoti ya mkaguzi inayojumuisha maoni yetu. Uhakika wa kutosha ni kiwango cha juu cha uhakika lakini si dhamana kwamba ukaguzi uliofanywa kwa mujibu wa ISAs utabaini kosa kubwa kila linapokuwepo. Makosa yanaweza kutokana na udanganyifu au makosa na huchukuliwa kuwa ni makubwa ikiwa, kwa upande mmoja au kwa ujumla, yanaweza kutarajiwa kuathiri maamuzi ya kiuchumi ya watumiaji yanayofanywa kwa misingi ya taarifa hizi za fedha.

Kama sehemu ya ukaguzi kwa mujibu wa ISAs, tunatumia utaalamu wetu wa kitaaluma wakati wote wa ukaguzi. Pia tunafanya yafuatayo:

- Kubaini na kutathmini hatari za makosa makubwa katika taarifa za fedha, kusanifu na kufanya taratibu za ukaguzi zinazojibu hatari hizo, na kupata ushahidi wa ukaguzi wa kutosha na unaofaa kutoa msingi wa maoni yetu.

- Kupata uelewa wa udhibiti wa ndani unaohusiana na ukaguzi ili kusanifu taratibu za ukaguzi zinazofaa kulingana na mazingira, lakini si kwa madhumuni ya kutoa maoni juu ya ufanisi wa udhibiti wa ndani wa Mfuko.

- Kutathmini usahihi wa sera za kihasibu zilizotumika na mantiki ya makadirio ya kihasibu na maelezo yanayohusiana yaliyotolewa na Wakurugenzi.

- Kutoa hitimisho juu ya usahihi wa matumizi ya Wakurugenzi ya msingi wa uendelevu wa biashara (going concern), na kwa mujibu wa ushahidi uliopatikana, ikiwa kuna hali ya kutokuwa na uhakika inayoweza kuleta shaka kubwa juu ya uwezo wa Mfuko wa kuendelea.

- Kutathmini uwasilishaji, muundo, na maudhui ya taarifa za fedha, ikijumuisha maelezo ya ziada, na ikiwa taarifa za fedha zinaonesha hali halisi kwa namna inayofikia uwasilishaji wa haki.

Tunawasiliana na Wakurugenzi wa Meneja wa Mfuko kuhusu, pamoja na mambo mengine, upeo uliopangwa na muda wa ukaguzi pamoja na matokeo muhimu ya ukaguzi.

Ripoti ya Mahitaji Mengine ya Sheria na Udhibiti

Kama inavyotakiwa na Kanuni za Masoko ya Mitaji na Dhamana za mwaka 1997, tunaripoti kwenu kwamba:

- **i.** Tumepata taarifa na maelezo yote ambayo kwa uelewa na imani yetu yalikuwa muhimu kwa madhumuni ya ukaguzi wetu, na kwa maoni yetu, taarifa za fedha zimeandaliwa ipasavyo kwa mujibu wa mahitaji ya kanuni;
- **ii.** Watu wote waliohusika na uendeshaji wa Mfuko wametenda kama inavyotakiwa na kwa muujibu wa mahitaji ya kanuni husika.
- **iii.** Vitabu na kumbukumbu sahihi zimewekwa na Mfuko na hesabu zinaendana na kumbukumbu za kihasibu za Mfuko;

- **iv.** Tumepata taarifa na maelezo ambayo, kwa uelewa na imani yetu, ni muhimu kwa madhumuni ya ukaguzi wetu;
- **v.** Ripoti ya Wakurugenzi inaendana na taarifa za fedha.

4. TAARIFA YA HESABU ZA MFUKO

TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI (STATEMENT OF INCOME OR LOSS AND OTHER COMPREHENSIVE INCOME) KWA MWAKA UNAOISHIA

31 DESEMBA 2025

	2025 TSH
Mapato yatokanayo na riba	1,979,414,663
Mapato mengineyo	2,131,997,400
Jumla ya Mapato	**4,111,412,063**
Gharama za Meneja	-353,182,725
Gharama za Mwangalizi wa Mfuko	-27,167,902
Gharama nyinginezo za Uendeshaji	-190,175,314
Jumla ya Gharama za Uendeshaji	**-570,525,941**
Ongezeko la Thamani kwa Wenye Vipande kabla ya kodi	3,540,886,123
Kodi ya Zuio	-13,776,125
Mapato halisi baada ya Kodi	**3,527,109,997**
Mapato mengineyo (other comprehensive income)	-
Ongezeko halisi la thamani ya Mfuko	**3,527,109,997**

URARI WA HESABU ZA MFUKO (BALANCE SHEET) MNAMO 31 DESEMBA 2025

	2025 TSH
Rasilimali za Mfuko	
Fedha Taslim	439,049,815
Amana katika Mabenki	4,500,942,708
Dhamana za Serikali	22,741,396,546
Rasilimali Nyinginezo Ambazo Hazijalipwa (Other Receivable)	79,355,778
Jumla ya Rasilimali	27,760,744,847
Dhima ya Mfuko	
Dhima Nyinginezo	-592,851,385
Jumla ya Dhima ya Mfuko	-592,851,385
Thamani Halisi ya Mfuko	**27,167,893,463**
Inawakilishwa na:	
Thamani Halisi ya Mfuko	**27,167,893,463**
Idadi ya Vipande	221,848,265.76
Thamani ya Vipande	122.46

TAARIFA YA MABADILIKO YA THAMANI YA MFUKO (STATEMENT OF CHANGES IN NET ASSETS ATTRIBUTABLE TO UNIT HOLDERS) KWA MWAKA ULIOSHIA 31 DESEMBA 2025

	2025 TSH
Thamani ya mfuko Awali	**0**
Mabadiliko/Ongezeko La thamani ya mfuko	3,527,109,997
	3,527,118,479
Miamala (Transactions) ya wenye vipande kwa mwaka	
Mauzo ya vipande (Sales)	28,008,657,167
Ununuzi ya vipande (Repurchase)	-4,367,873,702
Mabadiliko ya thamani ya mfuko	**23,640,783,465**
Thamani halisi ya Mfuko	**27,167,893,463**

TAARIFA YA MTIRIRIKO WA MAPATO (CASH FLOW STATEMENT) KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2025

	2025 TSH
FEDHA ITOKANAYO NA SHUGHULI ZA UENDESHAJI	
Ongezeko la Thamani (Mapato) baada ya Kodi	3,527,109,997
Imerekebishwa na:	
Faida/(Hasara) Mapato mengineyo (other comprehensive income) kwenye Hisa zilizosajiliwa DSE na Dhamana za serekali	-811,600,680
Faida/(Hasara) itokanayo na uwekezaji kwenye dhamana za Serikali	-1,809,153,412
Faida kabla ya mabadiliko ya Mtaji wa uendeshaji:	**906,355,905**
Mabadiliko ya Mtaji wa uendeshaji	
Amana za muda maalum katika taasisi za kifedha	
Ongezeko /(Kupungua) kwa Dhamana za serikali	-20,664,195,865
Ongezeko /(Kupungua) kwa dhima	592,851,385
Ongezeko /(Kupungua) kwa Hisa	-1,265,600,000
Fedha iliyotumika kwenye shughuli za uendeshaji	-20,430,588,576
Mapato yaliyopokelewa kwenye uwekezaji wa dhamana za serikali	1,729,797,634
Fedha halisi iliyotumika kwa shughuli za uendeshaji	**-18,700,790,942**
AMANA YA MFUKO (FINANCING ACTIVITIES	
Mauzo ya Vipande (Sales of Units)	28,008,657,167
Ununuzi (Repurchase) wa Vipande	-4,367,873,702
Fedha halisi iliyotokana na miamala ya wenye vipande	**23,640,783,465**
Ongezeko/(Punguzo) halisi la Fedha	**4,939,992,523**
Salio la fedha mwanzoni mwa Mwaka	**0**
Salio la fedha mwishoni mwa Mwaka	**4,939,992,523**

....
Mwenyekiti wa Bodi
Tarehe:23 Februari, 2026

....
Mkurugenzi
Tarehe: 23 Februari, 2026

5. TAARIFA YA MENEJA KUHUSU UWEKEZAJI

TAARIFA YA MENEJA KUHUSU UWEKEZAJI

1. Kuanzishwa kwa Mfuko

Timiza Fund ni mfuko wa uwekezaji wa pamoja unaosimamiwa na kampuni ya Zan Securities Limited. Mfuko huu uliidhinishwa rasmi na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) nchini Tanzania mnamo tarehe 16 Aprili 2024, baada ya kutimiza mahitaji yote ya kisheria na kikanuni yanayohusu uendeshaji wa mifuko ya uwekezaji wa pamoja.

Mfuko ulizinduliwa rasmi kwa umma mnamo tarehe 27 Mei 2024, ukiwa na lengo la awali la kukusanya kiasi cha TZS bilioni 10 katika mauzo ya awali. Katika kipindi hicho cha mauzo ya awali, Mfuko ulifanikiwa kukusanya TZS bilioni 10.38, ikiwa ni sawa na 103.8% ya lengo la awali. Hii ilionyesha mwitikio mkubwa na shauku ya wawekezaji katika aina hii ya uwekezaji

2. Tathmini ya Mfuko (Uendeshaji hadi mwaka 2025)

Kwa mujibu wa ripoti ya kwanza ya mwaka ya utendaji, Timiza Fund imeonyesha ukuaji endelevu wa thamani:

- Thamani Halisi ya Mfuko (NAV): Iliongezeka kutoka takriban TZS bilioni 10.38 mwezi Julai 2024 hadi kufikia TZS bilioni 27.1 ifikapo tarehe 31 Desemba 2025. Hii ni sawa na ongezeko la takriban 161% ya thamani ya jumla ya Mfuko katika kipindi hicho.

- Thamani ya Kipande: Bei kwa kila kipande iliongezeka kutoka TZS 100.00 hadi takriban TZS 122.4616, ikionyesha wastani wa ongezeko la 22.4616% kwa kila kipande tangu kuanzishwa kwa Mfuko.

Chati 1: Mwenendo wa NAV kwa kila Kipande na Ukubwa wa Mfuko wa TIMIZA tangu Kuanzishwa hadi 31 Desemba 2025



Mfuko wa Timiza Fund umeendelea kusimamia rasilimali zake kwa umakini na kimkakati, kulingana na sera ya uwekezaji na miongozo ya mfuko. Mchanganuo wa uwekezaji (portfolio) kufikia tarehe 31 Desemba 2025 ulikuwa kama ifuatavyo:

Chati II: Mchanganuo wa Uwekezaji wa Timiza Fund kufikia tarehe 31 Desemba 2025



Kutokana na Chati II, inaonekana wazi kuwa Dhamana za Serikali za muda mrefu (Treasury bonds) za vipindi tofauti zilichukua sehemu kubwa zaidi ya uwekezaji kwa 74%, zikifuatiwa na akaunti za amana za muda mfupi (call account) kwa 16%, na uwekezaji katika hisa zilizoorodheshwa sokoni kwa 8%. Mgawanyo huu mkubwa katika dhamana za serikali unasaidia kuhakikisha utulivu wa mfuko na mapato endelevu kupitia mzunguko wa fedha unaotabirika na faida nzuri.

Jedwali I: Mapato ya Mwaka na Ukubwa wa Mfuko wa Timiza kwa mwaka unaoishia tarehe 31 Desemba 2025

Na	*Mwaka*	*Ukubwa wa Mfuko (TZS Billion)*	*Faida*	*Faida linganishi (Benchmark)*
01	*2025*	*21.7*	*15.032%*	*11.4%*

3. Mazingira ya Kiuchumi nchini Tanzania

3.1 Pato la Taifa (GDP) na Mfumuko wa Bei (Uchumi wa Tanzania 2025)

Katika mwaka 2025, uchumi wa Tanzania uliendelea kukua kwa kasi ya wastani huku mfumuko wa bei ukidhibitiwa vizuri. Takwimu rasmi zinaonyesha kuwa Pato la Taifa (Real GDP) lilikua kwa takriban **5.9%** ikilinganishwa na mwaka uliopita, kikichochewa na uzalishaji katika sekta za kilimo, ujenzi, biashara, na huduma. Ukuaji huu umechanigwa na juhudi za Serikali katika kukuza miradi ya kimkakati pamoja na mazingira wezeshi yalioyoongeza uwekezaji wa sekta binafsi.

Mfumuko wa bei uliendelea kupungua na kubaki chini ya malengo ya kisera, ukiwa na wastani wa takriban 3.1% – 3.3% katika mwaka 2025, ambapo ni ndani ya kiwango cha kisera cha Benki Kuu ya Tanzania na unaoendana na malengo ya ustahimilivu wa bei. Ustahimilivu huu wa bei unasaidia mazingira mazuri ya uwekezaji kwa mifuko kama Timiza, kwani mfumuko wa bei wa chini una matokeo chanya kwenye thamani ya mali na faida za wawekezaji.
Uchumi thabiti na mfumuko mdogo wa bei hutoa mazingira wezeshi kwa mipango ya uwekezaji wa pamoja, kwani husaidia kuzuia mmomonyoko mkubwa wa thamani ya dhamana za uwekezaji unaosababishwa na mfumuko wa bei. Hii inajenga msingi imara wa ukuaji wa mapato na faida kwa wawekezaji.

3.2 Sekta ya Benki

Sekta ya benki nchini Tanzania ilibaki kuwa thabiti na ya kuvutia katika mwaka wa fedha wa 2025. Benki Kuu ilizingatia sera makini ya fedha, viwango vya riba vilidhibitiwa, na mfumo wa malipo ya kidijitali uliendelea kuenea kwa kasi. Amana na mikopo kwa sekta binafsi viliongezeka, huku benki zinazofanya vizuri zikiimarisha upatikanaji na ufanisi wa huduma kwa wateja.

Kwa mifuko ya uwekezaji wa pamoja kama Timiza, uthabiti wa sekta ya benki ni muhimu kwa sababu Mfuko huwekeza kwa kiasi kikubwa katika dhamana salama kama hati fungani za Serikali Sekta imara ya benki huchangia katika usalama wa fedha za wateja, hurahisisha ufanisi wa miamala, na huchangia ushirikiano kati ya benki na mifuko ya uwekezaji wa Pamoja kwa huduma kama vile ununuzi na uuzaji wa vipande.

3.3 Hali ya Kifedha

Nafasi ya Tanzania upande wa nje ilibadilika huku nakisi ya urari wa sasa (current account deficit) ikipungua hadi **2.2%** ya Pato la Taifa, kiwango cha chini zaidi katika kipindi cha miaka mitano. Mabadiliko haya yalitokana na mauzo ya nje ya dhahabu, mazao ya kilimo, na utalii, pamoja na kupungua kwa bei ya mafuta duniani. Akiba ya fedha za kigeni ilifikia **USD bilioni 6.3**, inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kwa miezi **4.9**, kiwango ambacho kiko juu ya hitaji la miezi 4.0. Deni la Taifa kwa uwiano wa Pato la Taifa (NPV) lilipungua hadi **40.6%** kutoka 41.1% katika kipindi kilichopita.

3.4 Sera ya Fedha na Mazingira ya Uchumi Jumla

Katika sehemu kubwa ya mwaka 2025, Kamati ya Sera ya Fedha ilihimili Riba ya Benki Kuu (CBR) katika asilimia **5.75**. Riba ya soko la fedha la mabenki kwa siku 7 (7-day interbank rate) iliongozwa ndani ya kiwango cha asilimia 3.75 hadi 7.75, ikionyesha msimamo thabiti wa kifedha uliolenga kudumisha upanuzi wa uchumi huku kukiwa na udhibiti wa mfumuko wa bei ndani ya lengo la asilimia 3–5.

Mfumuko wa bei kwa mwezi Desemba 2025 ulikua asilimia **3.6**, ukiwa ndani ya lengo.

Mazingira ya uchumi yaliendelea kuwa wezeshi:

- Ukuaji mkubwa wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia **20.3**.
- Mikopo chechefu (NPLs) ikiwa katika asilimia **3.1**, kiwango ambacho kiko chini kabisa ya ukomo wa juu.
- Akiba ya fedha za kigeni ya **USD bilioni 6.3**, inayotosheleza miezi **4.9** ya uingizajia bidhaa.
- Kushuka kwa thamani ya sarafu kwa asilimia **1.6** pekee katika mwaka 2025.
- Deni la taifa lilipungua kidogo hadi asilimia **40.6** ya Pato la Taifa (kwa msingi wa NPV).

Tanzania Bara ilirekodi ukuaji wa Pato la Taifa (Real GDP) wa asilimia **5.9** mwaka 2025, ikiwa ni chini kidogo ya makadirio ya asilimia 6.0. Ukuaji huo uliungwa mkono na sekta za kilimo, madini, na ujenzi. Uchumi wa Zanzibar ulikua kwa takriban asilimia **6.8**, ukichochewa na ujenzi, utalii, na viwanda.

Nakisi ya urari wa sasa ilipungua hadi asilimia **2.2** ya Pato la Taifa, kiwango chake cha chini kabisa katika miaka mitano, ikisaidiwa na mauzo madhubuti ya nje (dhahabu, utalii, kilimo) na bei ya chini ya mafuta.

4. Masoko ya Mitaji

Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) lilifunga mwaka 2025 kwa rekodi ya juu ya mtaji wa soko kufikia TZS trilioni 24, kiwango cha juu zaidi cha thamani katika historia yake. Hali hii ilichangiwa na misingi imara ya kiuchumi, ukuaji mkubwa wa gawio, mageuzi ya kimfumo ya soko, na kuongezeka kwa ushiriki wa wawekezaji wadogo kupitia mifumo ya kidijitali.

Mwaka huu uliashiria mabadiliko ya kimfumo katika masoko ya mitaji nchini Tanzania, yaliyodhihirishwa na kuimarika kwa ukwasi, mfumo bora ya upatikanaji wa bei za hisa, kuongezeka kwa dhamana zilizoorodheshwa, na ushiriki mkubwa wa wawekezaji wadogo.

4.1 Utendaji wa Soko la Hisa

Jumla ya mtaji wa soko ulifikia TZS trilioni 24 mnamo Desemba 2025, ikiwa ni thamani ya juu zaidi katika historia ya DSE. Mtaji wa soko la ndani ulifunga ukiwa na TZS trilioni 15.6. Soko lilifuata mwelekeo mzuri katika mwaka huo mafanikio ya taratibu katika miezi mingi, kushuka kidogo mnamo robo ya tatu (Q3), na kuimarika kwa nguvu kuelekea mwishoni mwa mwaka.

- Kielelezo cha Hisa Zote cha DSE (DSEI) kilipanda kwa asilimia 29.08 hadi kufikia pointi 2,761.93.
- Kielelezo cha Hisa za Ndani (TSI) kiliongezeka kwa asilimia 24.70 hadi pointi 5,759.41, vyote vikifunga katika rekodi za juu.

Soko la hisa liliongoza kwenye sekta ya benki na fedha, ambapo Kielelezo cha Benki, Fedha na Uwekezaji (BI) kilipanda kwa asilimia 88.46, kikichochewa zaidi na mapato makubwa na ukuaji wa gawio katika benki za CRDB na NMB. Kielelezo vya Viwanda na Huduma za Kibiashara vilishuka kufuatia mabadiliko ya sheria za utendaji wa soko za Juni 2025 yaliyoboresha ugunduzi wa bei na kurekebisha hisa za makampuni makubwa ambayo awali yalikuwa na ukwasi mdogo kama vile TBL, TCC, na Vodacom.

Ununuzi na uuzaji wa hisa

Mauzo ya hisa yalifikia **TZS bilioni 663.75** mwaka 2025, ikiwa ni ongezeko la asilimia **190.3** ikilinganishwa na mwaka uliopita. Idadi ya hisa zilizouzwa iliongezeka zaidi ya mara mbili hadi kufikia hisa milioni **477.81**, ongezeko la asilimia **109.57** ikilinganishwa na mwaka 2024. Kasi iliongezeka baada ya mabadiliko ya sheria za soko ya Juni 2025, yalio badilisha taratibu wa upatikanaji wa bei za kufungia soko za **wastani (volume weighted price)** hali iliyoboresha kwa kiasi kikubwa ukwasi wa soko. Kushuka kwa faida ya hati fungani za serikali pia kulihamasisha wawekezaji kuhamisha uwekezaji wao kwenda kwenye hisa, hususan hisa za benki ambapo faida ya jumla ilizidi asilimia **20–30**.

Ongezeko la Wawekezaji Wadogo

Ukuaji wa soko wa mwaka 2025 uliongozwa zaidi na wawekezaji wadogo (retail). Mfumo wa ununuzi na uuzaji wa hisa kupitia simu za mkononi (**DSE Mobile Trading Platform**) ulirekodi mauzo ya **TZS bilioni 106.68**, ikichangia asilimia **47.16** ya mauzo ya kawaida ya soko (bila kujumuisha mauzo ya jumla/block trades). Hili lilikuwa ongezeko la asilimia **656** ikilinganishwa na mwaka uliopita. Wawekezaji kupitia simu waliongezeka hadi **47,483** kutoka 8,795 mwaka 2024.

Gawio za hisa

Ongezeko wa gawio ulikuwa kichocheo muhimu zaidi nyuma ya mafanikio ya soko ya mwaka 2025. Makampuni kadhaa yaliyoorodheshwa yalitoa ongezeko kubwa la gawio:

- TBL iliongeza gawio kwa asilimia 134
- Vodacom iliongeza kwa asilimia 69
- TPCC (Twiga Cement) iliongeza kwa asilimia 54
- CRDB iliongeza kwa asilimia 30
- NMB iliongeza kwa asilimia 19

Soko lilibadilika kutoka hali ya uhaba wa ukwasi na kuwa soko linalotoa faida halisi ya fedha taslimu kwa wanahisa. Ongezeko la viwango vya gawio, hususan katika TBL, Vodacom, na TPCC, yaliimarisha imani ya wawekezaji kwa kiasi kikubwa.

Hisa zilizopata ongezeko kubwa la bei walichochewa zaidi na:

- benki zilizoorodheshwa kupata faida kubwa
- Kuimarika kwa shughuli za soko kulikonufaisha kampuni ya DSE Plc yenyewe.
- Marekebisho ya bei na kuongeza ukwasi

Ongezeko la wa Wawekezaji

Jumla ya akaunti mpya za CDS 123,547 zilifunguliwa mwaka 2025, ongezeko la asilimia 316 kutoka mwaka 2024. Jumla ya akaunti za CDS zilifikia 740,639 ifikapo mwisho wa mwaka. Inafurahisha kuona kuwa asilimia 40.33 ya wawekezaji wapya walikuwa na umri kati ya miaka 21 na 30, ikionyesha kuwa kundi la wawekezaji vijana wanaotumia teknolojia linaingia katika masoko ya mitaji. Mfumo wa biashara wa simu uliongeza wawekezaji wapya 94,805, na kufanya jumla ya akaunti za MTP kufikia 139,971, ikiwa ni asilimia 18.89 ya akaunti zote za CDS.

Kuorodheshwa kwa Dhamana mpya za uwekezaji

Mwaka 2025 ulikuwa mwaka wa kihistoria kwa uorodheshaji mpya na shughuli za kukusanya mitaji.

- Uorodheshaji wa Hisa na ETF: Mfuko wa kwanza kabisa wa ETF uliorodheshwa mnamo Oktoba 2025, ukikusanya kiasi kilichozidi lengo lake kwa asilimia 36 na kufikia mtaji wa soko wa TZS bilioni 21.3 ifikapo mwishoni mwa mwaka.

- Tanga Cement (TCCL): Walikamilisha zoezi kubwa zaidi la kutoa haki ya ununuzi wa hisa (rights issue) katika historia ya DSE, wakikusanya TZS bilioni 203.7.

4.2 Sukuk na Hati Fungani za Makampuni

Benki ya CRDB ilitoa Al Baraka Sukuk, ikikusanya mitaji katika sarafu ya Shilingi (TZS) na Dola ya Marekani (USD). Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pia ilitoa awamu mbili za Sukuk zenye thamani ya zaidi ya TZS bilioni 164 na USD milioni 80.7.

Hati fungani kadhaa za makampuni ziliorodheshwa mwaka 2025, zikiwemo:

- **Azania Bank** – Bondi Yangu
- **CRDB** – Samia Infrastructure Bond
- **NBC** – Twiga Bond
- **Stanbic Bank Tanzania** – Awamu mbili za uwekezaji
- **Tanzania Commercial Bank** – Stawi Bond
- **NMB** – Jamii Bond

4.3 Utendaji wa Soko la Hati Fungani za Serikali

Soko la Awali (Primary Market) Minada ya awali ilivutia maombi ya TZS trilioni 11.2 dhidi ya TZS trilioni 4.4 zilizotolewa, ikionyesha mahitaji makubwa huku wastani wa maombi ukizidi kiasi kilichohitajika kwa mara 2.31 (bid cover). Wawekezaji waliwekeza zaidi katika hati fungani za muda mrefu, hususan za miaka 15, 20, na 25, ambazo zilichangia asilimia 65 ya kiasi cha maombi yote. Faida (yields) ilishuka kwa kiasi kikubwa katika vipindi vyote; faida ya hati fungani ya miaka 25 ilishuka kutoka 15.84% katika robo ya kwanza (Q1) hadi 13.2% ifikapo robo ya nne (Q4).

Soko la Upili (Secondary Market) Mauzo ya hati fungani za serikali katika soko la upili yalifikia TZS trilioni 5.89. Hati fungani za miaka 10, 15, 20, na 25 zilichangia zaidi ya asilimia 91 ya mauzo yote. Faida jumuishi (yield curve) ulishuka kwa kiasi kikubwa, ambapo faida ya hati fungani ya miaka 25 ilipungua kutoka 15.24% (Q1) hadi 12.61% (Q4).

4.4 Soko la Upili la Hati Fungani za Makampuni

Uuzaji na ununuzi wa hati fungani za makampuni ilifanyika kwa hatifungani chache. Ambapo Hati fungani ya CRDB Samia Infrastructure Bond pekee ilichangia asilimia 35 ya biashara zote za hati fungani za makampuni. Hati fungani zote zilizoorodheshwa na CRDB kwa pamoja zilichangia takriban asilimia 63.8 ya mauzo ya hati fungani za makampuni. Ukwasi bado ni mdogo ikilinganishwa na soko la hati fungani za serikali, lakini kasi ya utoaji inaonyesha kuongezeka kwa ushiriki wa taasisi.

4.5 Mwenendo wa Soko la Kikanda

Kwa kipimo cha Dola ya Marekani (USD), Tanzania ilitoa faida ya asilimia 27.5 mwaka 2025, ikishika nafasi ya kati kati ya masoko ya Afrika. Malawi na Ghana zilifanya vizuri zaidi katika kanda hiyo, huku Mauritius ikirekodi utendaji duni.

4.6 Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja (CIS) nchini Tanzania

Hali ya Soko kufikia tarehe 31 Desemba 2025

1. Muhtasari wa Sekta

Hadi tarehe ya ripoti hii, Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja (CIS) nchini Tanzania inaendelea kuwa kama muhimu ya ya masoko ya mitaji, ikiwapa wawekezaji wadogo na wa taasisi fursa za uwekezaji zinazosimamiwa kitaalamu. Mifuko inayopatikana sokoni kwa kiasi kikubwa ni:

- Mifuko ya Soko la Fedha (Money Market Funds)
- Mifuko ya Uwiano (Balanced Funds)
- Mifuko ya Hisa (Equity Funds)
- Mifuko ya Mapato ya Kudumu/Hati Fungani (Fixed Income/Bond Funds)

Mifuko hii inadhibitiwa chini ya ungalizi wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) na inaendeshwa na mameneja wa mifuko na wadhamini wenye leseni.

TIMIZA FUND

2. Idadi ya Mifuko

Hadi tarehe 31 Desemba 2025, Tanzania ina mifuko 13 ya uwekezaji wa pamoja inayosimamiwa kikamilifu. Mifuko hii inasimamiwa na mameneja tofauti, huku mingi ikijikita katika dhamana za muda mfupi (money market funds) kutokana na upendeleo wa wawekezaji katika kulinda mtaji na upatikanaji wa ukwasi.

3. Jumla ya Dhamana Zinazosimamiwa (AUM)

Jumla ya dhamana zote zinazosimamiwa (AUM) katika mifuko yote ya uwekezaji wa pamoja ilifikia takriban: TZS Trilioni 4.35 (Jumla ya Sekta) Hii inaonyesha ukuaji endelevu wa mifuko ya pamoja, ukichochewa na:

- Kuongezeka kwa ushiriki wa wawekezaji wadogo.
- Faida shindani ikilinganishwa na amana za benki.
- Kuongezeka kwa uelewa wa uwekezaji
- Ushiriki wa taasisi (mifuko ya hifadhi ya jamii, makampuni, na vyama vya ushirika).

Mifuko inayowekeza kwenye dhamana za muda mfupi (money market funds) inashikilia sehemu kubwa zaidi ya sekta hii AUM, ikichangia zaidi ya 70% ya rasilimali za sekta hiyo.

4. Wastani wa Ukuaji wa Mwaka (YTD)

Wastani wa faida ya mwaka (YTD) katika mifuko yote ulikuwa takriban: 8% – 12% (Wastani wa Ukuaji wa Sekta) Mchanganuo kwa makundi:

- Mifuko ya Soko la Fedha: 8% – 11%
- Mifuko ya Hati Fungani: 9% – 12%
- Mifuko ya Uwiano: 10% – 15% (ikinufaika na kupanda kwa hisa)
- Mifuko ya Hisa: 20%+ (ikionyesha utendaji mzuri wa DSE mwaka 2025)

5. Maendeleo muhimu

- **A. Kuongoza kwa Mifuko ya dhamana za muda mfupi:** Sekta inaendelea kuongozwa na mahitaji ya ukwasi. Wawekezaji wanapendelea hatari ndogo, urahisi wa kutoa fedha, na faida endelevu
- **B. Kuongezeka kwa Ushiriki wa Wawekezaji Wadogo:** Mifumo ya kidijitali na usajili kupitia simu umerahisisha upatikanaji. Ongezeko la wawekezaji vijana linatarajiwa kunufaisha sekta hii zaidi.
- **C. Mazingira ya Faida ya Hati Fungani:** Kushuka kwa faida ya hati fungani za serikali mwaka 2025 kumeongeza thamani ya mifuko (NAV) kwa mifuko ya hati fungani na kuhamasisha uwekezaji kwenye hisa.
- **D. Ushiriki wa Taasisi:** Mifuko ya hifadhi ya jamii na makampuni zinaendelea kuwa wadau muhimu katika mifuko ya uwekezaji wa pamoja

TIMIZA FUND

6. Umuhimu Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja kwa Masoko ya Mitaji

Sekta ya Mifuko ya uwekezaji wa pamoja ina jukumu muhimu katika:

- Kukuza ujumuishi wa kifedha.
- Kuelekeza akiba za jamii kwenye masoko ya mitaji.
- Kuchangia upatikanaji wa mitaji kwa kampuni na taasisi mbali mbali
- Kuboresha ukwasi wa soko.

Ingawa sekta hii bado ni ndogo ikilinganishwa na sekta ya benki, kasi ya ukuaji inaashiria kuimarika kwa mfumo wa masoko ya fedha nchini Tanzania.

6. AZIMIO LA MKUTANO MKUU

Azimio la Mkutano Mkuu wa Wawekezaji wa Mfuko wa Timiza unaazimia kuipokea na kuikubali Taarifa ya Mwaka ya Mfuko wa Timiza ikiwemo Taarifa ya Hesabu za Mfuko wa Timiza kwa kipindi kilichoishia tarehe 31 DESEMBA 2025.

ZAN SECURITIES LIMITED
1st Floor, VIVA Tower,
Ali Hassan Mwinyi road
P.O. Box 5366
Dar es Salaam - Tanzania
Tel: +255 222 103 433
Mobile: +255 750 011 250
E-mail: info@zansec.co.tz
Website: www.zansec.co.tz

Zan Securities Limited
Timiza Fund
Dar Es Salaam: 1 st Floor, VIVA Towers, Ali Hassani Mwinyi Road, P.O. Box 5366,
Zanzibar: 3 rd Floor, Michenzani Mall, Karume Road
Tel: +255 222 103 433, Mobile: +255 750 011 250
www.zansec.co.tz, info.dsm@zansec.co.tz